KATIBA

# Profesa Maina auponda muundo wa Bunge la Katiba

**Ni ule wa kuchagua wajumbe 116 katika Bunge maalumu la Katiba.**

Fidelis Butahe, Mwananchi

**Dar es Salaam.** Mwanasheria maarufu, Profesa Chris Peter Maina ameuponda muundo wa Bunge la Katiba la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kushauri utizamwe upya kabla ya kufanyika kwa kura ya maoni mwakani.

Profesa huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, alisema kama hilo lisipofanyika inaweza kupatikana Katiba Mpya yenye mlengo wa chama kimoja cha siasa na kufafanua kuwa tatizo hilo limetokana na upungufu katika sheria ya mabadiliko ya Katiba ambayo imefanyiwa marekebisho kidogo na kupitishwa na wabunge mjini Dodoma wiki iliyopita.

"Vyama vya siasa vinaweza kujipanga na kuweka watu wao katika zile nafasi 166 za wawakilishi wa kawaida katika Bunge maalumu la Katiba, hapohapo kumbuka kuwa wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar wanaingia katika Bunge hilo," alisema.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Kiislamu Tanzania (Juwakita), Shamim Khan akichangia hoja kwenye warsha ya kujadili Rasimu ya Katiba Mpya iliyoandaliwa na Jukwaa la Katiba Dar es Salaam jana. **Picha na Fidelis Felix.**

Wakati Profesa Maina akieleza hayo, Mjumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na Mhadhiri wa Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), Profesa Palamagamba Kabudi alisema, kazi ya tume hiyo itaishia katika Mabaraza ya Katiba na kwamba katika hatua nyingine za Bunge la Katiba na kura ya maoni haitahusika.

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Bunge la Katiba litakuwa na wabunge 604 na wawakilishi 81 ambapo uwakilishi mkubwa utatoka katika vyama vya siasa huku CCM wakiwa na wabunge 398 sawa na asilimia 66 na upinzani wabunge 206 sawa na asilimia 34.

Alhamisi iliyopita wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), walipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Mpya, muswada ambao haukuungwa mkono na wabunge wa vyama vya Chadema, CUF na NCCR-Mageuzi kwa madai kuwa umejaa makosa mengi.

Kambi ya upinzani walitaka muswada huo usitishwe,huku wabunge wa CCM wakipinga,hali ambayo iliibua vurugu.

Wapinzani walikuwa wakipinga mambo kadhaa ikiwa ni kutokushirikishwa katika kutoa maoni kwa Wazanzibari na suala la Rais kupewa madaraka ya kuteua wajumbe wa Bunge maalumu la Katiba.

Akizungumza jana katika kongamano la Katiba lililoandaliwa na Jukwaa la Katiba (Jukata), Profesa Maina alisema ikiwezekana wabunge wanatakiwa kuelimishwa juu ya ushiriki wao katika bunge hilo ili watambue kuwa wanachokwenda kukifanya siyo kwa ajili ya kuwaondoa wao bungeni, bali ni kwa ajili ya Tanzania ya zaidi ya miaka 50 ijayo.